

9 Chukua hatua

Hatua na njia za haraka ambazo zitasaidia kuyalinda mazingira, kila siku!

1 Mazingira na uendelevu – Environment & sustainability

- Fuata Mazoezi ya Kimazingira (ECO-Practice) wakiti wote (angalia sehemu ya mbele ndani ya kitabu hiki)
- Kila mara unapofanya maamuzi ambao unaweza kuathiri mazingira, jiulize mwenyewe kama mazingira yatakuwa mazuri au mabaya ikiwa kila mtu atafanya uamuzi, na kuchagua chaguo endelevu
- Zungumza na rafiki zako na familia juu ya mazingira na kwa nini kuhifadhi kuna umuhimu
- Jaribu kununua bidhaa ambazo zimetengenezwa na vikundi vidogo vidogo vya wanawake ili kuwapa moyo

2 Bioanuai – Biodiversity

- Usiwaweke wanyama pori wadogo ikiwa ni pamoja na kasuku na kima, au samaki wa kuwindwa
- Epuka na ukataji wa miti, na kununua bidhaa ambazo zimetokana na mbao ambazo zimo hatarini kuisha, chagua mbao ambazo zina matumizi endelevu nazo ni mbao za minazi au za matunda kutoka kwenye mabustani badala yake
- Usinunue bidhaa ambazo zimetengenezwa kwa wanyama hatarini mfano pembe
- paka wako ametolewa uzazi
- Kuhamisisha wanyama pori kwa kuotesha miti asilia
- Punguza kuwepo kwa kunguru: hakikisha unatupa taka hasa taka za vyakula, ambapo hawawezi kufikia
- Siku ambazo za matembezi Zanzibar, saidia biashara za jamii na utembelee sehemu zilizoanzishwa hifadhi
- Ambazo zinapunguza athari za kimazingira na kusaidia kulinda wanyama pori
- Siku ambazo utakuwa kwenye matembezi kisiwa cha Zanzibar, jaribu kuwasaidia kuwahamasisha wafanyabiashara wa ndani ya jamii, na kutembelea hifadhi ambayo inapunguza madhara juu ya mazingira na zinasaidia kulinda wanyamapori

3 Mikoko – Mangroves

- Usikate mikoko kwa ajili ya kuni, chagua njia mbadala ambazo zinapatikana na endelevu
- Nunua mbao na karatasi zinazotokana na vyanzo endelevu
- Badilisha karatasi, kadi, kununua bidhaa ambazo zimebadilishwa kutokana na karatasi
- Tumia pande zote mbili za karatasi na rejea kutumia bahasha kwa matumizi mengine

4 Nyasi ya bahari – Seagrass

- Usiwachie boti yako au nanga ikaharibu nyasi bahari
- Usiokote changarawe au sheli, au kuchukuwa mawe au mchanga kutoka kwenye fukwe kwa ajili ya kujengea

5 Miyamba ya matumbawe – Coral reefs

- Usijaribu kutupa takataka au uchafu, hasa katika au karibu na bahari
- Usichukue au kununua kombe au matumbawe
- Jaribu kuuliza vipi samaki ambao umenunua wamevuliwa kwa njia zipi na usinunue samaki ambao wamevuliwa kwa mabomu / baruti

6 Uvuvi – Fisheries

- Angalia nyakati ambazo zimefungwa kwa ajili ya ukusanyaji wa kombe
- Chagua dagaa endelevu: kula madema au mishipi ya jadi ya kuvulia samaki kutoka kwenye hifadhi endelevu, epuka kula aina samaki ambao wapo hatarini kupotea kama vile papa, paa au pono
- Usijaribu kukusanya au kununua viumbe vya baharini kama vile konokono kwa ajili yakumbukumbu ya utalii!

7 Uchafuzi wa mazingira – Pollution

- Tupa takataka na uchafu wa majumbani sehemu ambazo zinatambulika, hasa plastiki: kupunguza, tumia upya, badilisha upya
- Rekebisha gari yako endapo itatoa harufu mbaya au moshi mweusi
- Kupunguza matumizi ya madawa makali na epusha katika uchafuzi wa mitaro ya maji na vianzio vya kusambaza maji safi
- Panda nafaka za chakula kwa mbolea ya samadi na mbolea ya asili jiepuse na madawa makali ya kuulia wadudu
- Tumia choo ambacho ni safi na salama kwa mazingira –sio katika fukwe!
- Epukana na uhifadhi mbaya – chukua mkoba au kikapu wako maalum wa kuhifadha matunda na mbogamboga utakapoenda sokoni
- Jaribu kutengeneza mbolea ya mboji kwa mabaki ya vyakula ambavyo vinaoza na majani
- Usiache vioo ambavyo vimevunjika-ni hatari vinaweza kumkata mtu na kusababisha hat kuwaka kwa moto
- Tupa betri vizuri ambazo hazitumiki tena
- Usitupe take katika fukwe, bahari au sehemu yeyote

8 Mabadiliko ya hali ya hewa – Climate change

- Hifadhi nishati: zima taa na umeme ambao utakuwa hutumii na tumia balbu ambazo hazitumii umeme mwangi
- Pika chakula haraka haraka, ili utumie nishati ndogo, na tumia chombo ambacho kitapitisha joto haraka kwa ajili ya kupikia
- Jaribu kutumia usafiri wa kawaida, au tembea kuliko kuendesha gari, pendelea kusafiri kwa njia ya majini kuliko angani
- Hifadhi maji: chemsha kadri upendavyo, na usiwache mifereji wazi yakamwaga maji – kosha vyombo na mbogamboga kwenye chombo chenye maji, usikoshe kwenye maji ambayo yanatiririka kwenye mifereji
- Chagua miti ambayo inastahmili hali ya ukame, hii inamaanisha ya kwamba uhitaji kumwagilia maji

10 Istilahi

- Anga** – Tabaka za gesi katika dunia
- Bahari kuu** – Maji ya bahari amabyo yapo mbali na nchi kavu na ya kina kirefu
- Baruti** – Ulipukaji wenye nguvu; au uvuvi haramu wa kulipua
- Bustani** – Shamba ambalo majani (nyasi) huota
- Chombo** – Mashine ya umeme ya nyumbani, k.m. mashine ya kufulia, simu za mikononi
- Gesi zinazoathiri hali ya hewa** – Gesi inayochangia katika kupata joto dunia kutokana na gesi inaokusanya joto kutoka kwenye jua, kama dioksidi ya kaboni na mitheni
- Ghuba** – Eneo la bahari lililozungukwa na ardhi / nchi kavu pande tatu
- Kitalu cha nyasi bahari** – Eneo la mchanga au tope ambapo nyasi bahari zinaota
- Kujikimu** – Hali ya kuwa na vitu vya kutosha unavyohitaji ili kukuwezesha uishi, lakini huna cha kuweka
- Kuogelea kwa kioo** – Ni kuogelea kwa kutumia kioo na mrija wa kuvutia hewa
- Kupauka kwa matumbawe** – Mchakato ambao kwake **polipu** wa matumbawe hutoa nje kutoka kwenye chembe chembe zao za maisha (seli) **mwani mdogo** zenye rangi joto linapozidi
- Latitude** – Masafa kutoka Kaskazini au Kusini ya Ikweta
- Mabadiliko** – Mchakato ambao kwake mimea na wanyama hubadilika ili kuweza kukabiliana na mazingira mapya
- Mabaki ya fueli** – Mafuta tyaliyofanyika chini ya ardhi kutokana na mabaki ya mimea na wanyama mamilioni ya miaka iliyopita, mfano gesi, makaa ya mawe na mafuta ya petroli
- Maji kujaa na kupwa** – Kupanda na kushuka kwa kawaida kwa viwango vya bahari vinavyotokana (mara mbili kwa siku) na mvuto wa graviti wa mwezi (na jua)
- Makazi** – Ni eneo ambalo mnyama au mmea unaishi
- Mbegu za mikoko** – Kipande cha mmea kinachovunjika na kuota mmea mwengine, kama miche ya mkoko inayochipua juu ya mti huo kabla ya kuanguka
- Mbolea** – Iliyofanywa kutokana na mimea iliyoza na uchafu wa wanyama – Iliowekwa kwenye chungu cha mbolea
- Mwamba wa matumbawe** – Mwamba uliopo chini yamaji uliofanywa kutokana na mifupa ya maelfu ya makoloni ya matumbawe hai na sponji
- Mwani mdogo** – Mimea yenye seli moja ambayo inaishi katika tishu za wanyama kama matumbawe, ambayo ina kitu chenye rangi kinacho ipatia rangi mimea
- Pangaboi** – Sehemu ya mota inayozunguka yenye viwembe viwili au zaidi, ambayo inazunguka katika maji au hewa kuifanya mashua au ndege iende
- Polipu** – Mnyama mdogo sahili wa majini kama anemone, ambaye amehusiana naye kwa karibu (sana)
- Polisterini** – Plastiki nyepesi yenye mapovu ya hewa, inayotumika kuhifadhia na kulinda vitu dhaifu, au huwekea vitu moto au baridi
- Rasi** – Eneo la bahari ambalo limetenganishwa na bahari kuu kwa mwamba (= mstari wa mawe, mchanga au matumbawe ambao upo kwenye maji ya kina kidogo)
- Rizomu** – Kigogo cha baadhi ya mmea vinavyoota kulalo juu au chini ya ardhi na inayotoa mizizi na majani
- Shimo** – Kuondoa takataka nyingi kwa kuzizika, au mahali ambazo takataka huzikwa
- Spishi** – Kundi la vitu vinavyoishi (ambavyo vinaweza kuwa aina ya mnyama, mmea, fangasi au bacteria) ambao wanafanana na wanaweza kuzaliana wenyewe kwa wenyewe lakini si pamoja na wengine wa makundi mengine
- Spishi adimu** – **Spishi** inyoishi mahali maalum tu
- Sunami** – Wimbi kubwa sana la uharibifu linalosababishwa na mtetemeko wa chini ya ardhi au mwendo wa dunia
- Tia nanga** – Kuifunga mashua, ngalawa ili ibaki mahali pamoja
- Tia rangi ya hudhurungi** – Kubadilisha ngozi ya wanyama kuwa ngozi ya kutumiwa kwa kutumia dawa ya kuhifadhiwa / kupaka rangi ili isiharibike kama vile magome ya mikoko
- Toweka kabisa** – Mchakato ambapo **spishi** hufa kabisa na haonekani tena
- Uchimbaji** – Utoaji wa rasilimali kama mawe na metali kutoka ardhini
- Ufukwe** – Kishorobo cha nchi kavu kwenye ukingo wa bahari, ziwa, au mto mpana; fukwe zinaweza kuwa za mchanga, mawe au tope
- Usanidi mwanga** – Mchakato ambao mmea hutumia nishati inayotoka kwenye mwanga wa jua kuzalisha chakula chake.